East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature

OPEN ACCESS

*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya

Volume-7 | Issue-2 | Feb- 2024 | DOI: 10.36349/easjehl.2024.v07i02.005

**Original Research Article**

# Ubainifu wa Matendo ya Kisihiri: Mifano Kutoka Bunilizi Teule za Fasihi ya Kiswahili ya Watoto

Gloria Kimbi[1*], Dkt, Edith Lyimo[1], Dkt, Grace Minja[1]

[1]Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Article History**
**Received:** 06.12.2023
**Accepted:** 14.01.2024
**Published**: 14.02.2024

**Journal homepage:**
https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Sihiri ni miongoni mwa mbinu zinazotumika katika utunzi wa kazi za kifasihi zikiwamo bunilizi za watoto za fasihi mbalimbali ulimwenguni. Aidha, kumekuwa na mkanganyiko mkubwa juu ya matumizi ya matendo [1]. ya kisihiri katika bunilizi za watoto. Wataalam wengi wa fasihi ya watoto wamechunguza fantasia kwa upekee wake bila kujadili matendo ya kisihiri kimajumui. Suala hili limesababisha kutokuchunguzwa kwa matendo mengine yanayohusisha sihiri na kuacha ombwe la maarifa juu ya matendo ya kisihiri yanayounda kazi mbalimbali za watoto na fasihi ya Kiswahili ya watoto ikiwemo. Hivyo, makala hii imebainisha na kufafanua matendo ya kisihiri yanayopatikana katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Ili kufanikisha lengo la makala hii, bunilizi tano za fasihi ya Kiswahili ya watoto ambazo ni *Mfalme Ndevu na Masikini-Mkatakuni*, *Sinderela*, Hadithi ya *Morile*, *Hadithi za Kusisimua* na *Marimba ya Majaliwa* zimechunguzwa. Data za makala hii zimekusanywa kutoka katika bunilizi teule kwa njia ya usomaji na uchambuzi matini. Nadharia ya Uhalisiajabu imeongoza ukusanyaji na uchanganuzi wa data za makala hii. Msingi wa nadharia uliotumika ni ule unaoeleza kuwa Uhalisiaajabu hutokana na muunganiko wa masuala halisi pamoja na yale yasiyo halisi. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto zimeundwa kwa matendo mbalimbali ya kisihiri. Matendo hayo yamegawanyika katika makundi matatu. Kundi la kwanza linahusisha matendo ya kimazingaombwe kama vile viumbe wasio binadamu kuzungumza, viumbe kujibadilisha muonekano na kuchukuwa sura na umbo la viumbe wengine, mtu kutumia vitu kujipatia mahitaji yake, vifaa visivyo rasmi kwa shughuli ya usafiri kutumika katika usafiri pamoja na fimbo kuchapa bila kushikwa na mtu. Kundi la pili linahusisha matendo ya kitabiri kama, mtu kutabiri mipango ya maadui kwa mtendwa na mtu kuteguwa kitendawili kabla ya kukisikia. Aidha, kundi la tatu limehusisha matendo ya kiganga kama vile dawa kutumika kama kinga dhidi ya maadui, mtu kutumia dawa kufichua siri ya mtu dhidi ya maadui zake pamoja na mtu kutumia dawa kumfufuwa ndugu yake. Aidha, makala hii imefafanua matendo husika ya kisihiri kama yalivyojitokeza katika bunilizi teule za makala hii.

**Keywords:** Sihiri Na Fasihi ya Watoto.

**Copyright © 2024 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 UTANGULIZI

Suala la sihiri katika fasihi ya watoto kimajumui limekuwa likijadiliwa na wataalam mbalimbali wa fasihi ya watoto kama vile Fox (2006), Subbotsky (2010), na Gavin (2021). Wataalam hao wanakubaliana kuwa sihiri ni mbinu muhimu katika ujenzi wa mtindo wa kazi mbalimbali za watoto. Kwa

[1] [1]Sihiri hudhihirika kupitia matendo yanayolenga kupata uhakika WA masuala mbalimbali. Aidha, matendo ni mbinu ya msingi inayotumiwa na wasihiri katika shughuli zao na ndiyo huukilia usihiri pamoja na ubobezi wa msihiri. Bila matendo sihiri haiwezi kudhihirika (Ericcsson, 2009 Na Subbotsky 2014). Hivyo, katika makala hii matendo ya kisihiri yaliyochunguzwa Ni yale tu yaliyobainika katika bunilizi teule za utafiti huu. Matendo husika ni matendo ya kimazingaombwe, matendo ya kitabiri pamoja na matendo ya kiganga.

***Corresponding Author:** Gloria Kimbi
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

mfano, Fox (2006) anaeleza kuwa sihiri ni mbinu ya utunzi wa kazi za watoto ambayo hutumika kwa watoto mapema sana katika umri wa utoto na huwasaidia watoto katika makuzi yao kama vile kujua masuala mbalimbali ya kimaisha na kiulimwengu. Subbotsky (2010) na Gavin (2021) wanafafanua zaidi kwamba, matendo ya kisihiri ni dira katika utunzi wa bunilizi za watoto na hutumika kuwaelekeza watoto namna ya kuishi, kukabiliana na mazingira yanayowazunguka na kuufurahia ulimwengu kwa namna yao. Kutokana na maelezo ya wataalam hawa ni wazi kuwa sihiri ni mbinu muhimu katika ujenzi wa bunilizi za watoto. Hii ni kwa sababu bunilizi za watoto zimetungwa na zinaendelea kutungwa kwa matendo ya kisihiri. Aidha, utafiti wa makala hii umebaini kuwa licha ya matendo ya kisihiri kuonekana kama mbinu muhimu ya utunzi wa bunilizi za watoto, bado matendo husika ya kisihiri hayajawekwa bayana. Hii ni kwa sababu hakuna utafiti uliobainisha matendo ya kisihiri katika bunilizi za watoto. Kutokana na hayo, makala hii inaweka bayana matendo mbalimbali ya kisihiri yanayotendeka katika bunilizi teule za watoto. Hii itawasaidia watunzi wa kazi za watoto kuelewa aina ya matendo ya kisihiri ambayo huwafaa watoto kulingana na uelewekaji wake unaotokana na urazini wa watoto kama hadhira ya kazi husika.

Vilevile, sihiri katika fasihi ya Kiswahili ya watoto imechunguzwa kwa mawanda finyu. Kwa mfano wataalam wa fasihi ya Kiswahili ya watoto kama vile Bakize (2012); Bakize, Lyimo na Ngugi (2019) wamechunguza fantasia katika bunilizi za watoto za Kiswahili. Fantasia ni mtindo wa uwasilishaji wa kazi za kisanaa unaohusisha matukio, wahusika na mandhari ya ulimwengu mwingine, yaani ulimwengu usioonekana wala kufikika na wenye mambo tofauti na ulimwengu halisi (Cahill, 2012 na Mahmood, 2020). Aidha, makala hii inatambua fantasia kama miongoni mwa matendo ya kisihiri. Hivyo, kuna ombwe la maarifa katika ubainishaji wa matendo ya kisihiri katika bunilizi za watoto na fasihi ya Kiswahili ikiwemo. Pengine hii ndiyo sababu iliyowafanya wataalam wa fasihi ya Kiswahili ya watoto kuchunguza fantasia kwa upekee wake kana kwamba ndiyo matendo pekee ya kisihiri katika kazi za watoto. Kwa kuwa fantasia hufanyika katika ulimwengu dhahania, makala hii imebainisha matendo ya kisihiri yanayotendeka katika ulimwengu halisi yanayopatikana katika bunilizi teule za fasihi ya Kiswahili ya watoto. Aidha, makala hii imegawanywa katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza Ni utangulizi ambao unaeleza madhumuni ya makala hii. Sehemu ya pili inaelezea Nadharia iliyoongoza uchambuzi WA data. Sehemu ya tatu inafafanua methodolojia za utafiti. Sehemu ya nne ni uchambuzi wa data na sehemu ya tano ni hitimisho.

**2.0 Nadharia ya Uhalisiajabu**

Uchambuzi wa data za makala hii umeongozwa na nadharia ya Uhalisiaajabu iliyoasisiwa na Franz Roh mwaka (1925) na kutumika zaidi katika sanaa ya uchoraji. Nadharia hii ilihusishwa kwa mara ya kwanza na fasihi ya Amerika ya Kusini na Gabriel Garcia (1927). Kipindi hiki kinajulikana kama awamu ya kwanza ya matumizi ya Nadharia ya Uhalisiajabu. Aidha, Nadharia hii iliendelea kutumika huko Amerika ya Kati miaka ya 1940 kama awamu wa pili. Awamu ya tatu ilianza huko Amerika ya Kaskazini na maeneo mengine duniani miaka ya 1960. Nadharia hii imekuwa ikitumika katika kazi mbalimbali za kifasihi (Anne, 1994 ; Faris, 2004). Wataalam hao wanaeleza kuwa Nadharia ya Uhalisiajabu hueleza namna masuala halisi yanavyohusishwa na yale yasiyo halisi katika kutekeleza suala fulani. Wanafafanua zaidi kuwa, uhalisiajabu hutumika kuvunja mpaka uliopo kati ya masuala halisi na yasiyo halisi na hivyo kumwezesha mtunzi wa kazi ya kifasihi kujifaragua na kutoa ujumbe na maonyo mbalimbali kwa kutumia matendo mbalimbali ya kisihiri. Kwa kuwa sihiri ni sehemu ya utamaduni, matendo ya kisihiri hutumika kuwasilisha masuala muhimu yanayopatikana katika jamii. Lengo huwa kuifunza, kuifurahisha na kuikemea jamii juu ya masuala fulani yanayokiuka kanuni na taratibu za jamii. Nadharia hii ina misingi sita. Msingi uliotumika ni ule unaoeleza kuwa upatikanaji wa matendo ya kiuhalisiajabu huhusisha muunganiko wa masuala halisi na yale yasiyo halisi kulingana na mtazamo ama mazoea ya kijamii. Msingi huu umetuongoza kubainisha matendo ya kisihiri yanayopatikana katika bunilizi tulizoziteua.

## 3.0. METHODOLOJIA YA UTAFITI

Data za makala hii zimepatikana kwa kusoma matini teule kisha kuzichanganua kwa kutumia mkabala wa maelezo. Bunilizi zilizochambuliwa ni pamoja na *Mfalme Ndevu na Masikini-Mkatakuni* ya Abdallah (1995), *Sinderela* ya Moshi (1995), *Morile* ya Mariki (2004), *Hadithi za Kusisimua* ya Mzindakaya (2005) na *Marimba ya Majaliwa* iliyoandikwa na Semzaba (2008). Bunilizi hizi zilipatikana kwa kutumia usampulishaji lengwa. Ziliteuliwa kwa sababu zimesheheni matendo mengi ya kisihiri. Aidha, mbinu ya kusimba maudhui ilitumika kwa kutathmini jinsi matendo yalivyotendeka.

**4.0 Matendo ya Kisihiri Yaliyojitokeza katika Bunilizi Teule**

Bunilizi teule za makala hii zimeundwa kwa matendo mbalimbali ya kisihiri. Matendo husika yamegawanyika katika makundi matatu ambayo ni mazingaombwe, utabiri na uganga.

**4.1 Matendo ya Kisihiri ya Mazingaombwe**

Mazingaombwe ni mchezo wa kugeuza hali fulani ili iweze kuonekana kinyume na uhalisia na kuwahadaa watu kwa kutumia nguvu za miujiza (Penegyres, 2016). Vilevile, mazingaombwe ni hila, ujanja na ujuzi wa kumdanganya mtu ili aweze kuamini kuwa kitu au jambo fulani analoliona au kulisikia siyo kama lilivyokuwa awali (BAKITA, 2022). Kutokana na fasili za wataalam ni wazi kuwa mazingaombwe ni hali ya kutenda mambo mbalimbali yasiyo ya kawaida kwa namna ya kawaida. Utendaji husika hukamilika kwa msaada wa nguvu isiyo ya kawaida ambayo katika makala hii inarejelewa kama sihiri. Kwa mantiki hiyo ni

wazi kuwa matendo ya kisihiri hufanyika kwa namna ya kawaida licha ya kutokuwa halisi. Data za utafiti huu, zimeonesha kuwapo kwa matendo mbalimbali yafuatayo ya kimazingaombwe:

**4.1.1 Viumbe wasio Binadamu Kuzungumza**

Bunilizi teule za makala hii zimeonesha namna viumbe wasio binadamu walivyoweza kuzungumza kama binadamu. Mathalan, imeelezwa katika bunilizi ya *Mfalme Ndevu* namna gogo lilivyozungumza na binadamu. Tendo hilo lilifanyika msituni wakati Masikini-Mkatakuni alipokuwa anatafuta kuni za kuuza ili akidhi mahitaji yake. Mwandishi anaeleza:

… Akasikia gogo likisema; "Ni nani huyo?" Ni mimi. Masikini-Mkatakuni alalijibu. ... "Unataka nini?" Gogo likauliza. Natafuta kuni……Zunguka nyuma ya mbuyu ulioko mbele yako. Ukishafika nyuma ya mbuyu utamkuta kondoo umchukue. Chochote utakachomwambia akupatie atakupa. Gogo lilimweleza (Abdallah, 1995: 3).

Maelezo hayo yanaonesha namna gogo lilivyozungumza na Masikini-Mkatakuni ambaye ni binadamu na kumpa maelekezo ya namna ya kujipatia mahitaji yake kupitia kondoo. Beauclair (2014) anaeleza kuwa uwezo wa kuzungumza amepewa binadamu pekee. Sifa hii ndiyo inayotofautisha mawasiliano ya binadamu na viumbe wengine. Kitendo cha gogo kuzungumza kinakiuka uhalisia kwani gogo haliwezi kuzungumza wala kumwelekeza binadamu jambo lolote. Pia, katika bunilizi ya *Hadithi ya Morile* tumeelezwa namna kipande cha nyama kilivyozungumza baada ya kumezwa. Cora (1978) anaeleza kuwa nyama ni sehemu ya mwili wa mnyama inayotumika kama kitoweo. Kwa maelezo ya mtaalam huyo, kipande cha nyama hakiwezi kuzungumza. Licha ya hayo, katika bunilizi ya *Hadithi ya Morile* tumeelezwa kuwa kipande cha nyama kinavyozungumza. Mwandishi anaeleza:

Morile alipomeza tu kipande cha nyama alisikia sauti ikitoka tumboni mwake ikisema, "Morile umenila basi na wewe utaliwa (Mariki, 2004:21).

Maelezo hayo yanaonesha namna kipande cha nyama kinavyozungumza baada ya kufika tumboni kwa Morile. Tendo hili ni la kustaajabisha kwani kiuhalisia kipande cha nyama ya Ng'ombe hakiwezi kuzungumza. Ili tendo hilo liweze kufanyika ni lazima kuwe na sihiri. Aidha, kipande cha nyama ni kitu halisi kinachoweza kuonekana na kushikika. Tendo lisilo halisi ni nyama kuzungumza hivyo kuzalisha tendo la kisihiri aina ya mazingaombwe.

**4.1.2 Mfu kumtokea Mtu-hai katika Mazingira Halisi na Kumpa Maelekezo**

Mfu ni mtu aliyekufa, kimwili lakini katika ulimwengu wa roho huwa hai na huheshimiwa na wanajamii wake kama mhenga (Mbiti, 1967). Aidha, katika bunilizi ya *Sinderela* tunaelezwa namna bibi Sinderela, ambaye ni mfu anavyomtokea Sinderela katika mazingira halisi na kumsaidia kufika katika sherehe iliyokuwa imeandaliwa na mfalme wa nchi yao. Bibi huyo alimtokea Sinderela alipokuwa analia baada ya mama yake wa kambo pamoja na ndugu zake kuondoka na kwenda kwa mfalme kwa ajili ya sherehe na kumwacha mkiwa nyumbani. Mwandishi anasema:

Ghafla akatokea mama mmoja kutoka kwenye mawingu akamwambia Sinderela. "Usiogope mimi ni bibi yako wa zamani. Nimesikia kilio chako na nimekuja kukusaidia. Alimtengenezea gari la kumpeleka kwa haraka shereheni. Pia, aligeuza mavazi yake kuukuu na kuwa mapya na ya kuvutia (Moshi, 1995:10).

Maelezo hayo yanaonesha namna bibi Sinderela aliyekuwa mfu alivyofika mahali alipo mjukuu wake Sinderela. Baada ya kufika alimtengenezea Sinderela mavazi pamoja na chombo cha usafiri kilichomfikisha kwenye sherehe kwa muda mfupi. Pia, katika bunilizi ya *Marimba ya Majaliwa* tumeelezwa namna bibi Majaliwa alivyorudi duniani akiwa na umbo la kibinadamu ilhali alikuwa mfu. Alirudi kumsaidia mjukuu wake katika harakati za kusaka marimba yake yaliyoibwa na Kongoti. Kwa hakika matendo yaliyojadiliwa hapo juu yanathibitisha kuwa bibi Sinderela na bibi Majaliwa walikuwa na nguvu ya siri katika kutekeleza masuala waliyoyafanya. Nguvu husika ndizo zinazotambulika katika utafiti huu kama sihiri. Barley (2006) anaeleza kuwa sihiri huweza kutoka kwa Mungu, miungu na wahenga. Kutokana na hayo sihiri ya bibi Sinderela na bibi Majaliwa ilitoka kwa wahenga. Aidha, bibi kumsaidia mjukuu wake ni suala la kawaida. Suala lisilo halisi ni bibi aliyekufa kurudi katika mazingira halisi na kumsaidia mtu kutimiza malengo yake. Hivyo, masuala halisi na yasiyo halisi yameungana katika kukamilisha tendo la kisihiri linaloingia katika kundi la mazingaombwe.

**4.1.3 Kiumbe Kujibadili na Kuchukua Sura na Umbo la Kitu Kingine**

Sura katika makala hii ni muonekano wa ndani na nje wa kitu au kiumbe fulani (Wolff, 2010). Aidha, sura huweza kumtambulisha na kumtofautisha mtu na mtu au kiumbe na kiumbe. Hii ni kwa sababu kila mtu kaumbwa kwa sura na umbo la pekee tofauti na mwingine. Aidha, Wolff anafafanua zaidi kuwa, hakuna kiumbe chenye uwezo wa kujibadili jinsi kilivyoumbwa. Hali hii ni tofauti katika data za utafiti huu kwa sababu watu na viumbe mbalimbali wamejibadilisha na kuchukua sura na maumbo ya viumbe wengine. Kwa mfano, katika *Hadithi za Kusisimua* tumeelezwa namna simba alivyojibadilisha na kuwa binadamu. Simba ni mnyama jamii yap aka ambaye hula nyama (BAKITA, 2022). Kiuhalisia simba huishi porini na chakula chake kikuu ni nyama. Hutegemea kupata nyama kutoka kwa wanyama wengine wadogowadogo hususan swala. Licha ya hayo, data za utafiti huu zimeonesha namna simba alivyojibadilisha na kuwa na mwonekano wa binadamu. Pia, simba huyo akiwa porini kuwinda huchukua umbo na tabia za simba halisi. Mwandishi anasema:

Wakati wa mawindo shemeji wa Simbawazi alikuwa makini kumchunguza Simbawazi. Alishuhudia Simbawazi akijibadili umbo na kuwa simba halisi." Aliogopa lakini alijikaza ili aone hatma ya Simbawazi. Baada ya simba kumkamata swala kama kitoweo, alijibadilisha muonekano wa simba na kuwa binadamu (Mzindakaya, 2005:59).

Maelezo haya yanaonesha namna Simbawazi alivyojibadili umbo kutoka katika umbo la binadamu na kuchukua umbo la simba halisi. Tendo hili linastaajabisha kwa kuwa kiuhalisia hakuna kiumbe chenye uwezo wa kujibadili kuwa kiumbe kingine. Ili iwezekane ni lazima kuwepo na nguvu za ziada zipitazo zile za kihalisia. Nguvu husika ndizo zinazojulikana katika utafiti huu kama sihiri. Aidha, simba na binadamu ni viumbe halisi kabisa katika mazingira yetu. Lakini kitendo ya simba kujibadili muonekanao na kuwa binadamu si halisi. Kuungana kwa matendo hayo mawili kunazalisha tendo la sihiri la kimazingaombwe.

Pia, katika *Hadithi ya Morile* tumeelezwa juu ya mabadiliko ya kiazi kitamu kuwa mtoto wa binadamu. BAKITA (2022) inaeleza kuwa kiazi ni sehemu ya mzizi wa mmea ambayo imekuwa nene na huifadhi chakula cha mmea. Kutokana na hayo ni dhahiri kuwa kiazi ni chakula cha mmea lakini hutumika pia kama chakula cha viumbe mbalimbali hasa binadamu. Katika data za utafiti huu imebainika kuwa kiazi kimebadilika umbo lake na kuwa mtoto. Tendo hili lilitokea baada ya Morile kwenda pangoni kuangalia kiazi alichokificha siku moja akiwa anamsaidia mama yake kuchimba viazi. Mwandishi anasema:

Morile aliamka asubuhi na kwenda pangoni kuangalia kiazi alichokificha siku moja nyuma. Looh kwa mshangao alipofika pangoni alikuta kiazi kimebadilika na kuwa mtoto mzuri ajabu. Mtoto huyo alikuwa akilia sababu ya njaa (Mariki, 2004: 4).

Maelezo hayo yanaonesha tendo linalostaajabisha kwani kiazi hakiwezi kuwa mtoto wa binadamu. Kutokea kwa tendo hili kunahusishwa na nguvu za sihiri. Hoffman (1960) anaeleza kuwa, sihiri humpa mtu uwezo wa kujibadilisha kimuonekano na hata kitabia. Anafafanua zaidi kuwa, sihiri humwezesha mtu kujibadilisha na kuchukua muonekano wa viumbe wengine au vitu mbalimbali kama vile wanyama wa kutisha, mawe na hata maji. Mtu akishabadilika huchukua sifa za kiumbe mpya suala linalopoteza uhalisia na utambulisho wake. Maelezo haya yanathibitisha tendo la kisihiri kwa kiazi kujibadilisha muonekano wake na kuwa mtoto wa binadamu.

**4.1.4 Vyombo Visivyo Rasmi Kwa Ajili ya Usafiri Kutumika katika Usafiri**

Vogel (1974) anaeleza kuwa safari hujumuisha aina zote za mijongeo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Vegel anafafanua zaidi kuwa safari huweza kufanyika kupitia vyombo mbalimbali mahususi Kwa ajili ya shughuli hiyo. Anataja vyombo vya usafiri wa ardhini kama vile magari, treni, na kadhalika. Pia, anataja vyombo vya usafiri WA angani Kama ndege na meli kwa ajili ya majini. Kwa mantiki hiyo vifaa Kama pikipiki, magari, treni, meli na ndege ni vyombo ambavyo hutumika katika kukamilisha safari mbalimbali. Aidha, tofauti na maelezo hapo juu kuhusu vyombo rasmi vya usafiri, tumeelezwa katika bunilizi teule za utafiti huu namna watu walivyotumia vitu mbalimbali ambavyo si maalumu katika shughuli za usafiri. Mathalan, tumeelezwa namna mtu alivyotumia ufagio Kama chombo cha usafiri. Sullivan (1997) anaeleza kuwa ufagio Ni kifaa kinachotumika katika usafi wa sehemu mbalimbali za majumbani kama vile sakafu na mazingira yanayozunguka nyumba. Maelezo haya yanapishana na data za utafiti huu kwani katika bunilizi teule za utafiti huu tumeelezwa namna watu walivyotumia ufagio kama chombo cha usafiri. Kwa mfano, katika *Marimba ya Majaliwa* tumeelezwa namna bibi pamoja Na Majaliwa walivyosafiri kwa ufagio baada ya kutoka hotelini kujipatia chakula cha usiku. Mwandishi anaeleza:

… alipomaliza kufagia alitoka nje na ule ufagio akiwa ameambata na Majaliwa. Mara bibi aliukalia ule ufagio akiwa ameushika kwa mikono miwili. "Panda" akamwambia Majaliwa. Majaliwa alipanda katika ufagio kisha ukaruka juu kwa kasi. Kufumba na kufumbua walijikuta wako angani, mji mzima wa Zanzibar ukionekana mdogo mfano wa ramani kubwa (Semzaba, 2008:22 na 23).

Maelezo hayo yanaonesha namna bibi na Majaliwa walivyotumia ufagio kama chombo cha usafiri. Tendo hili linakiuka uhalisia kwa sababu ufagio hauwezi kutumika kama chombo cha usafiri kwani hauwezi kupaa angani. Pia, katika *Hadithi ya Morile* tumeelezwa namna kiti kilivyotumika kama chombo cha usafiri. Whiteley (1987) anaeleza kuwa kiti ni kifaa ambacho watu hutumia kukalia. Mara nyingi huwa na miguu minne ili kuweza kustahimili uzito wa mtu bila kuyumba. Katika bunilizi ya tajwa hapo tumeona kuwa kiti kimetumiwa na Morile kama chombo cha usafiri. Mwandishi anaeleza:

Morile alikiweka kiti katikati ya uwanja WA nyumba Yao Na kukikalia. Mara kiti kilianza kurefuka kwenda juu. Kilianza kupaa taratibu kuelekea mawinguni. Morile alipandishwa juu mpaka akapotea katika upeo wa macho kisha alipotea kabisa mawinguni. Baada ya muda kiti kilishuka na kijirudisha taratibu katika kimo chake cha awali (Mariki, 2004: 6 na 7).

Maelezo hayo yanaonesha namna Morile alivyopaa angani kwa kutumia kiti. Tendo hili linashangaza kwani katika hali ya kawaida kiti hakina

uwezo wa kupaa juu angani. Kufanyika kwa tendo hili kunadhihirisha kuwa kiti cha Morile kilikuwa na nguvu zipitazo zile za kiti cha kawaida. Aidha, kiti ni kifaa halisi kinachopatikana na kutumika katika mazingira yanayotuzunguka. Kitendo kisicho halisi ni kiti kumpaisha mtu kutoka ardhini kuelekea angani. Kuungana kwa masuala hayo mawili kunazalisha tendo la kisihiri la kimazingaombwe.

### 4.1.5 Mtu kutumia Viumbe Na Vitu mbalimbali Kujipatia Mahitaji yake

Katika bunilizi teule za utafiti huu tumeelezwa namna watu walivyokidhi mahitaji yao kwa kupata msaada kutoka kwa viumbe pamoja na vitu mbalimbali nje ya binadamu. Kwa mfano, katika *Marimba ya Majaliwa* tumeelezwa namna Majaliwa alivyotumia jiwe la rubi kuhamisha chakula kutoka kwa anayekula na kwenda tumboni kwake. Lombard (2005) anaeleza kuwa rubi ni jiwe la thanani. Ni madini adimu na ngumu inayopendeza kwa sababu ya uangavu na rangi yake. Lombard anaeleza pia kuwa, jiwe ni vipande vigumu vya miamba vipatikanavyo ardhini. Miamba hiyo hutumika kwa matumizi mbalimbali ya binadamu hasa kutengeneza samani na nyumba. Licha ya hayo, tumeelezwa katika bunilizi ya *Marimba ya Majaliwa* namna jiwe la rubi lilivyotumika kumpatia Majaliwa mahitaji yake. Bibi anamwambia Majaliwa:

Mjukuu wangu, unakumbuka jana nilikupa jiwe la rubi? Tia mkono mfukoni uliguse na useme: "njoo lakucha ulapi na kimasa" baada ya muda bibi yake alimuuliza. "Mjukuu wangu, nikuagizie nini? Majaliwa alimwambia bibi yake: "Nasikia nimeshiba kiwango cha kutaka kucheua. Tumbo limejaa hata kuhema ni tatizo" (Semzaba, 2008: 21 na 22).

Maelezo hayo yanaonesha namna bibi alivyomwelekeza mjukuu wake Majaliwa namna ya kushiba kwa kutumia jiwe la rubi. Alimwambia kila mara anapohitaji kula anapaswa kwenda sehemu ambapo watu wanakula, kisha ashike jiwe la rubi na kutamka majina ya vyakula wanavyokula watu wanaokula ili viingie tumboni mwake. Majaliwa alifanya kama alivyoelekezwa na bibi yake na ikawa hivyo. Chakula husika kiliingia tumboni kwa Majaliwa moja kwa moja bila ya kupitia mdomoni. Tendo hili linastaajabisha kwani mtu hawezi kushiba bila kula. Pia, chakula hupitia mdomoni kuingia tumboni. Vilevile, jiwe haliwezi kumpatia mtu chochote kwa kuwa si kiumbe hai. Aidha, kushiba ni jambo halisi ambalo hutokea kwa kiumbe hai baada ya kula. Mtu kushiba bila kula ni suala linalostaajabisha. Kutendeka kwa suala kama hili kunahitaji sihiri. Aidha, katika bunilizi ya *Mfalme Ndevu* tumeelezwa namna kondoo alivyompatia binadamu chakula. Abbott (2018) anaeleza kwamba kondoo ni mnyama afugwaye na binadamu ili atumike kama kitoweo ambacho kinaweza kuwa nyama, maziwa, mbolea na ngozi. Data za utafiti huu zimeeleza masuala mbalimbali yaliyotendwa na kondoo kinyume na uhalisia wa mnyama huyo. Mwandishi anaeleza:

…Gogo lilimwambia Masikini-Mkatakuni kuwa kondoo utakayemkuta nyuma ya mbuyu atakupatia unachohitaji. Masikini-Mkatakuni akamwambia kondoo "Nataka pilau nzuri." Palepale ikatokea pilau ikiwa kwenye sahani, akala na kushiba kisha akamchukua kondoo na kwenda naye nyumbani (Abdallah, 1995: 4).

Maelezo hayo yanaonesha namna Masikini-Mkatakuni alivyoweza kupata chakula kupitia kondoo. Tendo hili linastaajabisha. Pia, tendo hili limefanyika pale mke wa Masikini-Mkatakuni alipomwambia kondoo kuwa anahitaji chakula. Vilevile, watoto wa Mfalme Ndevu walipata chakula kupitia kondoo. Matendo haya yanathibitisha usihiri uliokuwa ndani ya kondoo.

### 4.1.6 Kifaa Kuchapa Watu Bila Kushikwa

Katika bunilizi ya *Mfalme Ndevu na Masikini-Mkatakuni* tumeelezwa namna fimbo ilivyochapa watu bila kushikwa na mtu. Dayle (1994) anaeleza kuwa fimbo ni kijiti kirefu kinachotumika kwa namna nyingi ili kufikia umbali kuliko mkono wa binadamu. Pia, fimbo hutumika kutoa adhabu kwa wakosaji hasa watoto. Kitendo cha fimbo kuchapa bila kushikwa wala kuwezeshwa kuchapa na mbinu zozote za kisayansi kimefanyika pale Masikini-Mkatakuni, watoto wa mfalme na Mfalme mwenyewe walipoiamuru fimbo kucheza. Kwa mfano, Mfalme anasema:

… fimbo cheza ngoma. Fimbo ilianza kwa kurukaruka kisha kuanza kumchapa mfalme harakaharaka na kwa nguvu sana. Iliendelea kumchapa mpaka akapiga kelele. "Nisaidieni, Nakufa!" Ilimchapa mpaka akazimia (Abdallah, 1995: 26).

Maelezo haya yanaonesha namna fimbo ilivyowachapa watu bila kushikwa na mtu wala kuwekwa kwenye mtambo maalum kwa ajili ya kuchapa. Ilianza kumchapa Masikini-Mkatakuni kisha mke wake, watoto wa mfalme na mfalme mwenyewe. Kitendo hiki ni cha kustaajabisha na kinakiuka uhalisia. Ili fimbo iweze kuchapa bila kushikwa au kuunganishwa kwenye mtambo maalum kunahitajika nguvu ambazo katika utafiti huu zinajulikana kama sihiri. Hivyo, kitendo cha fimbo kutandika watu bila kushikwa ni cha sihiri ya kimazingaombwe.

### 4.1.7 Wafu Kufufuliwa Na kuwa Hai Tena

Brody, (2016) anaeleza kuwa ufufuo ni hali ya mtu au kiumbe kuupata uhai tena baada ya kufa. Kamm (2017) anaeleza kuwa kifo ni mwisho wa uhai. Huwa ni mwisho wa michakato yote ndani ya kiumbe hai ambayo ni sababu ya uhai. Naye, Rowe (2000) anaeleza kuwa, kifo ni pale uhai unapoondoka ndani ya kiumbe hai chenyewe. Maelezo ya Kamm na Rowe yanaonesha kuwa mtu au kiumbe chochote kikifa hakiwezi kuwa hai tena. Aidha, katika bunilizi ya Hadithi za Kusisimua tumeelezwa kuwa mtu alikufa na kuzikwa kisha akafufuliwatendo hili lilifanywa na Ali Gombe kwa kaka yake Ali Simba. Mwandishi anasema:

… Ali Gombe alipofika kwa mfalme Daudi aliomba kuoneshwa mahali alipozikwa Ali Simba. Alipofika kaburini alipiga kaburi kwa fimbo mara tatu kisha akafukua na kutoa mwili wa Ali Simba. Alichemsha maji kisha akatia unga wa maini na kumkanda ndugu yake mwili mzima. Baada ya muda Ali Simba alisimama na kumkumbatia Ali Gombe kwa furaha huku machozi yakimtoka (Mzindakaya, 2005: 41).

Maelezo haya yanaonesha namna Ali Gombe alivyomfufua kaka yake Ali Simba. Tendo hili linapingana na uhalisia kwani mtu akifa hana uwezo wa kurudi na kuwa hai tena. Ili jambo hilo lifanyike ni lazima mtu husika awe na nguvu za kisihiri. Aidha, Ali Gombe alitegemea sihiri kutoka kwa wahenga. Kupitia sihiri hiyo, aliweza kumfufua kaka yake Ali Simba aliyefariki kwa kumrudishia uhai tena. Hili ni tendo la kisihiri la kimazingaombwe.

**4.1.8 Viumbe Kuingia Chumbani bila Kupitia Mlangoni**

Hill (2018) anaeleza kuwa chumba ni sehemu ya jengo kubwa inayowapa watu nafasi ya kutosha kwa shughuli fulani. Kwa mantiki hiyo chumba ni sehemu ndogo katika nyumba. Aidha, mlango ni sehemu maalumu ya kupitia ili kuingia au kutoka mahali (Clark, 2019). Kwa maelezo hayo tunaona kuwa mlango ni eneo maalumu kwa ajili ya kuingia au kutoka sehemu fulani. Katika data za utafiti huu tumeelezwa namna watu walivyoingia chumbani bila kupitia mlangoni. Tendo hili lilifanywa na Bibi kwa mjukuu wake Majaliwa. Bibi anamwambia Majaliwa:

Mjukuu wangu, naona umechoka sana na unahitaji kupumzika. Inabidi nikutafutie eneo la kulala. “Funga macho.” Majaliwa akafunga macho yake. “Yafungue” Majaliwa akayafungua na kushangaa. Alijikuta yuko hotelini katika chumba kimoja kizuri sana cha kulala. Majaliwa alikwenda mlangoni akaukuta umefungwa. Aliingilia wapi? Hakujua.Yeye alijikuta tayari yuko ndani!” (Semzaba, 2008:80 na 81).

Maelezo haya yanaonesha namna Majaliwa alivyoingia katika chumba cha hoteli bila kupitia mlangoni. Tendo hili linashangaza kwani ili mtu aingie ndani ni lazima apite mlangoni. Kitendo cha mtu kujikuta yuko ndani kinastaajabisha. Ili kifanyike ni lazima kuwe na sihiri. Aidha, kuingia chumbani ni ni suala halisi linalofanywa na watu kila mara. Kitendo kisicho halisi ni mtu kuingia chumbani bila kupita mlangoni. Kuungana kwa matendo tajwa hapo juu kunazalisha tendo la kisihiri la kimazingaombwe.

**4.1.9 Maiti Kukatwa Shingo Na Kupasuliwa Tumbo kisha Kurudi katika Hali yake ya Kawaida**

Fuss (2003) anaeleza kuwa maiti ni mwili wa mnyama aliyekufa. Kutokana na maelezo ya mtaalamu huyu tunaona kuwa ili mnyama na binadamu akiwemo aitwe maiti ni lazima awe hana uhai. Pia, kupasua ni tendo la kukata kitu na kukitenganisha kwa lengo la kuzalisha vipande zaidi ya kimoja (TUKI, 2014). Katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua* tumeelezwa namna maiti ya mtu ilivyotenganishwa shingo na kiwiliwili na baada ya muda viungo husika kuungana kana kwamba havikutenganishwa. Tendo hili lilitokea baada ya Mzee Ally kuwaambia wanawe kuwa, akifa wamkate shingo yake na kuitenganisha na kiwiliwili, kisha wapasue tumbo lake na kutoa ini ambalo aliwaelekeza kulikausha na kutumia unga wake kwa ajili ya kutengeneza dawa. Mwandishi anasema:

Mzee Ally aliwaita wanaye kuwaaga na kuwapa maelekezo mbalimbali. Baada muda mfupi alifariki. Watoto wa mzee Ally ambao ni Ali Gombe na Ali Simba walimkata baba yao shingo na mpasua tumbo kisha wakatoa ini na kulikausha. Lakini walipomaliza kazi hiyo tu maiti ya baba yao ilionekana kujiunga upya kama alivyowaeleza kabla ya kifo chake (Mzindakaya, 2005:10).

Dondoo hii inaelezea tendo la kutisha na kustaajabisha. Kiuhalisia mtu hawezi kutenganishwa kichwa na kiwiliwili kisha baada ya muda viungo husika vikaungana na kurudi kama vile havikukatwa. Halikadhalika, tumbo la binadamu haliwezi kupasuliwa na maini kutolewa kisha kuunga kama halijapasuliwa. Matendo kama haya huwezekana kwa msaada wa sihiri.

**4.1.9 Mtu Kupigwa Risasi Mfululizo bila Kujeruhiwa wala Kufa**

Risasi ni kifaa cha metali chenye umbo la mduara au mcheduara ambalo huwekwa ndani kwenye bunduki aghalabu kikiwa na baruti ili kiwe na mlipuko kinapofyatuliwa (BAKITA, 2022). Kwa mantiki hiyo ni wazi kuwa mtu akifyatuliwa au kujifyatulia risasi akiwa hajavaa vizuia risasi ni lazima aumie au pengine afe. Aidha, katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua* tumeelezwa namna mtu alivyofyatuliwa risasi bila kudhurika kwa namna yeyote. Tendo hili lilitokea pale askari wa mfalme Daudi walipokuwa wanataka kumuua Ali Simba. Mwandishi anasema:

Askari wa mfalme Daudi waliagizwa wamuue Ali Simba. WalimwamuruAli Simba kutoka nje. Alipotoka tu askari wale walimfyatulia risasi mfululizo. Watu walijua kuwa mkombozi wao ameuawa. Vilio vilisikika kila mahali. Kumbe hakuna hata risasi hata moja iliyompata wala kumjeruhi (Mzindakaya, 2005: 37).

Maelezo haya yanaonesha namna askari wa mfalme Daudi walivyomfyatulia Ali Simba risasi ishirini. Baada ya tendo hilo Ali Simba hakufa wala kupata jeraha lolote katika mwili wake. Kiuhalisia mtu akifyatuliwa risasi huumia vibaya na wakati mwingine hupoteza maisha. Aidha, mtu kufyatuliwa risasi ni tendo halisi linaloweza kufanyika katika mazingira yanayotuzunguka. Tendo lisilo halisi ni mtu kutodhurika baada ya kufyatuliwa risasi. Aidha, matendo ya kisihiri kama yalivyojadiliwa hapo juu yanaingia katika kundi la

matendo ya kisihiri ya kimazingaombwe. Sehemu inayofuata ni mjadala kuhusu tendo la pili la kisihiri ambalo ni utabiri.

### 4.2 Utabiri

Utabiri ni uwezo wa kujua matukio na matendo ya wakati ujao (Koch, 2015). Kwa mantiki hiyo, utabiri ni hali ya mtu kujua masuala mbalimbali yatakayotokea katika dakika, saa, siku au miaka ijayo. Hivyo, mtabiri ni mtu mwenye uwezo wa kujua masuala mbalimbali ya wakati ujao hata kabla hayajatokea. Katika sehemu hii tutafafanua matendo mbalimbali ya kitabiri kama yalivyojibainisha katika bunilizi teule za utafiti huu. Matendo husika ni kama yafuatayo:

#### 4.2.1 Mti Kutabiriwa Kuanguka Na Ikawa Hivyo

Laibson na List (2015) wanaeleza kwamba mti ni mmea ambao huweza kupandwa au kuota wenyewe. Aidha, mti ukikomaa hutumika kwa matumizi mbalimbali kama vile kutoa kivuli, mbao za kutengeneza samani na kuni. Katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisismua* tumeelezwa kuwa mti wa mlingoti ulitabiriwa kuanguka na baada ya muda alianguka. Aidha, mti husika ulianguka bila kuwa na changamoto zozote za kimazingira. Utabiri huu ulifanywa na Ali Simba alipokuwa anasafiri kuelekea kwa mfalme Daudi. Alimwambia Ali Gombe kuwa akiuawa kwa hujuma mti mkubwa wa mlingoti uliokua karibu na nyumba yao utang'oka. Baada ya Ali Simba kuuawa licha ya kwamba alikuwa mbali na nyumbani, mlingoti uling'oka. Mwandishi anasema:

Baada ya Ali Simba kuanza safari ya kuelekea kwa Mfalme Daudi, Ali Gome alibaki na wasiwasi mkubwa. Aliogopa kuwa kaka yake atauawa na joka. Alikumbuka naneno ya Ali Simba hivyo, alikuwa akiutazama mti wa mlingoti kila siku. Siku kaka yake alipouawa mlingoti uling'oka na kuanguka (Mzindakaya, 2005: 39).

Maelezo haya yanaonesha namna utabiri wa Ali Simba ulivyotimia. Kiuhalisia utabiri hufanywa na wanasayansi pamoja na watu wenye elimu ya unajimu. kKwa kuwa hatujaelezwa kuwa Ali Simba alikuwa mnajimu, tendo alikolifanya ni la kisihiri. Sihiri ya Ali Simba ilitoka kwa wahenga wake. Aidha, wahenga wa jamii ya Ali Simba walitoa sihiri iliyowasaidia watu wa jamaa yake kupambana na changamoto mbalimbali za maisha pamoja na kujilinda na matatizo mbalimbali ya kibinafsi na hata kijamii. Hivyo, Ali Simba kutabiri kung'oka kwa mlingoti na ukang'oka kweli ni tendo la kisihiri la kitabiri.

#### 4.2.2 Mtu Kutabiri Mipango ya Maadui Kwa Mtendwa

Kitendo hiki kimeelezwa katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua*. Katika hadithi hiyo Bi Sekela anatabiri mpango wa Maua na Joka dhidi ya mjukuu wake Furahisha hata kabla ya kutokea. Bi Sekela anamwambia Furahisha:

Mjukuu wangu, leo Maua na huyo Joka lake wamepanga kukuuwa. Utakaporejea kwako utapewa chakula lika kutengewa maji ya kunywa. Ukiomba maji utaambiwa uyafafuate mwenyewe. Joka atakuwa amejificha nyuma ya mtungi na atakuuma. Chukua huu upanga. Utauparaza katika mtungi na joka atatoweka (Mzindakaya, 2005:19).

Maelezo hayo yanaonesha namna Bi Sekela alivyotabiri mipango mibaya ya Maua na Joka dhidi ya mjukuu wake Furahisha. Kitendo hiki kilitokea kweli kwani Furahisha alipofika nyumbani alikuta mkewe Maua katenga chakula mezani bila kuandaa maji ya kunywa. Alipouliza kuhusu maji ya kunywa aliambiwa afuate mwenyewe. Furahisha alifuata maji huku akifuata maelekezo aliyopewa na bibi yake. Alipoutoa upanga na kuuparaza kwenye mtungi, joka kubwa liliibuka na kutimua mbio. Kitendo hiki kinaonesha kuwa Bi Sekela alikua mtabiri kwani jambo aliloliieleza lilitimia. Aidha, kitendo cha Bi Sekela kinadhihirisha kuwa alikuwa na sihiri iliyomfumbulia mambo mbalimbali. Kwa ujumla, katika sehemu hii tumefafanua matendo ya kisihiri ya kitabiri. Sehemu inayofuata imejadili data zinazohusu matendo ya kiganga yaliyojitokeza katika bunilizi teule za utafiti huu.

### 4.3 Uganga

Stokl, (2014) anaeleza kuwa, uganga ni elimu kuhusu tiba za magonjwa ya watu, wanyama, mimea, jinsi ya kuzuia magonjwa pamoja na kurudisha uzima. Anafafanua zaidi kuwa, uganga huweza kutumika kumkinga mtu na maadui. Pia, uganga huweza kupunguza au kuondoa nguvu ya kinga dhidi ya maadui. Kwa mantiki hiyo kazi kubwa ya uganga ni kutibu yaani kuondoa matatizo. Lakini huweza kutumika kinyume kuleta matatizo. Sehemu inayofuata inajadili matendo ya kiganga yaliyojitokeza katika bunilizi teule za utafiti huu.

#### 4.3.1 Matumizi ya Dawa kujikinga Na Maadui

Tendo hili lilifanywa na Ali Simba katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimuwa.* Ali Simba alitumia dawa ya kinga dhidi ya askari wa Mfalme Daudi waliotaka kumuua. Ali Simba alipopata taarifa juu ya kuuawa kwake alijiandaa. Mwandishi anaeleza:

Baada ya Ali Simba kupata taarifa kuwa anapaswa kuuawa alitahamaki lakini hakuwa na hofu sana. Hii ni kwa sababu alijua namna ya kujilinda. Aliutwaa upanga wake, akalamba ungaunga wa dawa yake, kisha akafungua mlango. Akasema, "Ewe upanga usiwaue hawa. Niokoe tu na maisha yangu. Wale askari waliduwaa. Badala ya kufyatua risasi wakaanguka chini. Miili yao ikawa mizito kama magunia ya chumvi. Hawakuweza kumdhuru Ali Simba (Mzindakaya, 2005:36).

Maelezo hayo yanaonesha namna Ali Simba alivyotumia uganga kujilinda dhidi ya maadui zake

ambao ni askari wa Mfalme Daudi. Dawa husika ilitengenezwa kwa kutumia maini ya baba yake yaliyochanganywa na unga wa sisimizi. Aidha, uganga hulenga kuponya au kumlinda mtu na maadui (Stokl, 2014). Kwa mantiki hiyo, tendo alilofanya Ali Simba ni la kiganga. Aidha, ili uganga ufanyike ni lazima kuwe na sihiri. Kwa mfano Ali Simba alipata sihiri ya kuwalegeza askari wa mfalme Daudi kwa kutumia upanga wa ajabu pamoja na dawa aliyoitengenezwa kutokana na maelekezo ya baba yake aliyekuwa marehemu. Hivyo, Ali Simba alifanya tendo la kisihiri la kiganga.

**4.3.2 Matumizi ya Dawa Kufichua Siri ya Mtu**

Tendo hili lilifanyika katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimuwa* na serikali ya mfalme Daudi dhidi ya Ali Simba. Baada ya askari wa Mfalme Daudi kushindwa kumuua Ali Simba, ilitaka kujua siri ya Ali Simba. Walimwagiza mganga mkuu wa nchi hiyo kutafuta chanzo cha nguvu za Ali Simba. Mganga wa Mfalme Daudi alitumia dawa na kugundua kuwa nguvu ya Ali Simba iko kwenye unga wa maini na sisimizi aliokuwa nao Ali Simba. Alitengeneza dawa itakayowasaidia kuchukua dawa alizokuwa akitumia Ali Simba kujikinga na maadui. Mganga mkuu wa nchi ya Mfalme Daudi anasema:

Atafutwe sisimizi mwenye kichwa kilicho upande, mguu mmoja na mkono mmoja. Pia, Panya maalumu atalishwa sisimizi huyo na atakwenda kukichukua kifurushi hicho na kukipoteza. Hapo Ali Simba anaweza kuuawa. Kila kitu kilifanywa kama alivyoelekeza mganga mkuu. Baada ya hapo kinga ya Ali Simba iliweza kuchukuliwa na panya na hakua na nguvu tena. Aliposhambuliwa kwa mara nyingine aliuawa (Mzindakaya, 2005: 38).

Maelezo hayo juu yanaonesha namna mganga wa mfalme Daudi ilivyotengeneza dawa ya kuiba kinga ya Ali Simba dhidi ya maadui zake. Baada ya kitendo hicho Ali Simba aliuawa. Masuala yote yaliyotendeka ni ya kiganga. Uganga uliohusika hapa ni wa kudhuru na ndiyo maana Ali Simba alifariki. Aidha, kutengeneza unga wa sisimizi kunaweza kutekelezeka katika mazingira yanayotuzunguka hivyo ni suala halisi. Jambo lisilo halisi ni panya kutumika katika shughuli ya wizi. Kuungana kwa masuala tajwa hapo juu kunazalisha tendo la kisihiri la kiganga.

**4.3.3 Matumizi ya Dawa Kufufua Wafu**

Ufufuko ni hali ya mwili kurudi kuishi baada ya kufa kwa mfano wa kuamka kutoka usingizini (Caldwell, 1910). Kwa mantiki hiyo, ufufuko ni hali ya mtu aliyekufa kurudi kuwa hai. Kwa kawaida mtu akishakufa hana uwezo WA kuwa hai tena. Maelezo haya yanatofautiana na masuala yanayopatikana katika bunilizi ya *Hadithi za Kusisimua* kupitia hadithi ya Kijana Shujaa. Tumeelezwa katika hadithi hii namna Ali Gombe alivyomfufua kaka yake Ali Simba baada ya kuuawa Kwa hila. Mwandishi anaeleza:

… Ali Gombe alichemsha maji kisha alitia ule unga wa maini na kumkanda nduguye. Robo saa baadaye, Ali Simba alisimama na kumkumbatia nduguye kwa furaha (Mzindakaya, 2005: 42).

Maelezo hayo yanaonesha namna Ali Gombe alivyotumia dawa kumfufua kaka yake Ali Simba. Ali Gombe alitumia unga wa maini na maji ya moto kumkanda kaka yake aliyekua marehemu. Suala hili liliwezekana kwa kuwa vijana hawa walilindwa na dawa zenye sihiri kutoka kwa baba yao. Hii inamaanisha kuwa sihiri ni mali ya jamii na huhusisha familia pana ya watu wanaoishi na wale waliokufa (Mbiti, 1969). Watu hao huhakikisha usalama wa mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Hivyo, matendo ya kiganga yanahusisha sihiri.

**4.4 Mjadala Mfupi**

Kazi mbalimbali za kifasihi zimeonekana kujengwa kwa kutumia matendo ya kisihiri. Bunilizi za watoto zimepewa upekee wa kunasibishwa na matendo ya kisihiri. Matendo husika ya kisihiri yametumika kama mbinu ya kisanaa inayoonesha ukomavu wa mwandishi katika dhana ya mwigo. Hii ni kwa sababu sihiri huwezesha utendekaji wa matendo ambayo kiuhalisia hayawezi kufanyika. Sihiri husika huiwezesha simulizi kutambaa na kufikia mawanda tarajiwa ya mwandishi. Kupitia sihiri mwandishi huwasilisha maudhui juu ya masuala yanayoikabili jamii hivyo walengwa wa kazi husika kupata ujumbe uliokusudiwa zaidi ya ambavyo angetumia matendo halisi pekee. Vilevile, matendo ya kisihiri katika kazi za watoto husababisha furaha miongoni mwa watoto ilikinganisha na ile waipatayo kutokana na matendo halisi. Hivyo, ni wazi kuwa matumizi ya matendo ya kisihiri katika utunzi wa kazi za watoto ni mbinu iliyozoeleka miongoni mwa watunzi wengi wa kazi za watoto. Suala la mjadala ni je, matendo ya kisihiri katika bunilizi za watoto husababisha mwitikio chanya pekee kwa hadhira yake lengwa ambao ni watoto? Kama siyo, nini athari hasi ya matendo ya kisihiri kwa watoto?

Aidha, tafiti ambazo si rasmi zinaeleza kuwa kuna baadhi ya kazi za watu wazima zimeundwa kisihiri. Suala hili ni geni na halijazoeleka miongoni mwa watunzi na hata hadhira ya bunilizi husika. Swali ni je, ujumbe wa mwandishi utaifikia hadhira tarajiwa ya bunilizi husika kama ilivyokusudiwa? Aidha, makala hii imebaini kuwa hadhira ya watoto hufurahia sana matendo ya kisihiri katika kazi zao. Je, hadhira ya watu wazima ina mapokeo gani juu ya matumizi ya matendo ya kisihiri katika kazi zao? Swali hili na maswali mengine ya mjadala katika makala hii yanahitaji majibu. Hivyo, tafiti mbalimbali zinapaswa kufanyika juu ya matumizi ya matendo ya kisihiri hasa katika kazi za watu wazima ili kujua faida na hasara ya mbinu husika katika kazi husika za kisanaa pamoja na hadhira yake.

**4.5 Hitimisho**

Makala hii imebaini kuwa bunilizi za watoto zimejengwa kwa matendo mbalimbali ya kisihiri kama vile mazingaombwe, utabiri na uganga. Matendo hayo yametumika kama mbinu ya kimtindo na kidhamira hivyo yamesaidia kuifikia ujumbe hadhira iliyokusudiwa. Pia matendo husika ya kisihiri yameonesha mfungamano mkubwa na matendo halisi. Aidha, imebainika kuwa matendo ya kisihiri ya kimazingaombwe ndiyo yaliyotamalaki bunilizi za watoto. Hii ni kwa sababu mazingaombwe huwafanya watoto kuwa sehemu ya utendaji wa suala linalotendwa hivyo watoto huburudika. Vilevile, mazingaombwe hufanyika kwa njia ya ubunifu kiasi cha watoto kuyaamini na kuyapenda sana. Jambo hili huwafanya watoto kushiriki katika kutenda matendo mbalimbali ya kimazingaombwe ama kwa kujua au kwa kutokujua. Kutokana na ushiriki wao, watoto hupenda matendo ya kimazingaombwe kwani huamini kuwa ni sehemu ya maisha yao.

## MAREJELEO


- Abdallah, K. (1995). *Mfalme Ndevu Na Masikini Mkatakuni*. Dar es Salaam: Readit Books Ltd.
- Anne, C. H. (1994). *Lies that Tell the Truth: Magic Realism Seen Through Contemporary Fiction from Britain*. New York: Amsterdam.
- Bakita. (2022). Kamusi Kuu ya Kiswahili (Toleo la 3). BAKITA, Tanzania.
- Bakize, L. H. (2012). “Fantansia Katika Fasihi ya Kiswahili Kwa Watoto”. *Kioo cha Lugha, 8,* 122-134.
- Barley, M. D. (2006). “The Meaning of Magic”: *In Magic Rituals and Witchcraft, 1*(1), 1-23. Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/24767701. Imesomwa tarehe 7/12/2022.
- Brody, B. (2016). Jewish Reflections on the Resurrection of the Dead. *The Torah U-Madda Journal*, 17:93-122. Inapatikana katika http://www.jstor.org/stable/26203062. Imesomwa tarehe 1/10/2023.
- Cahill, M. (2012). “The Role of Magic in Fantasy Literature: Exposing Reality through Fantancy”. *English*, *8*, 1- 44. Inapatikana katika https://scholarsarchive. library.albany.edu/honors .com. Imesomwa tarehe 12/11/ 2021.
- Clark, J. T. (2019). “The *Skene* Door in the Prologue of Sophocles’ *Ajax*.” *Mnemosyne*, *72*(5), 861- 866. Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/26787702. Imesomwa tarehe 6/3/2023.
- Cora, D. (1978) “Eating Meat and Eating People.” *Philosoph*, *3*(206), 465 - 497. Combridge University Press. Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/3749876. Imesomwa tarehe 4/12/2022.
- Doyle, C. C. (1994) “The Long Story of the Short End of The Stick.” *American Speech Spring*, *69*(1), 96 -101. Duke University Press. Inapatikana katika Https:// www.jstor.org/stable/455954. Imesomwa tarehe 5/12/2022.
- Faris, B.W. (2004). *Ordinary Enchantment Magical Realism and the Remistification of Arrative.* Nashville: Vanderbilt UP.
- Fox, J. (2006). *What Books About Magic do for Children-that Others Stories Can’t.* Oxford Children’s Books. Inapatikana katika https:/www.readbrightly.com. Imesomwa tarehe 4/6/2022.
- Fuss, D. (2003). “Corpse Poem.” *Critical Inquiry*, 30/30(1/1), 1- 30. Inapatikana katika : https://doi.org/10.1086/380805. Imesomwa tarehe 19/12/2022.
- Gavin, L. M. (2021). The Magic of Play: How it Inpires and Aids Early Development. Kidshealth. Inapatikana katika https://kidshealth.org/en/parents/play-magic.html. Imesomwa tarehe 10/12/2022.
- Hill, C. E. (2018). “Sources of Meaning in *Meaning in Life: A Therapist’s Guide. American Psychological Association*, 51- 62. Inapatikana katika. http://www.jstor.org/stable/j.ctv1chrz3w.8. Imesomwa tarehe 30/3/1023.
- Hoffman, D. G. (1960). “Jim’s Magic: Black or White?” *American Literature*, *32*(1), 47–54. Inapatikana katika https://doi.org/10.2307/2922801. Imesomwa tarehe 12/01/2023.
- Jarvie, I. C., & Agassi, J. (1967). “The Problem of Rationality of Magic.” *The British Journal of Sociology*, *18*, 55-74. Inapatikana katika https://www.Jstor.org/stable/588590. Imesomwa tarehe 1/11/ 2022.
- Kamm, F. M. (2017). “The Purpose of My Death: Death, Dying, and Meaning.” *Ethics*, *127*(3), 733-761. Inapatikana katika https://www.jstor.org/stable/26541041. Imesomwa Tarehe 3/2/2023.
- Koch, A. (2015). Alternative healing as magical self-care in alternative modernity. *Numen*, *62*(4), 431-459. http://www.jstor.org/stable/24644878.
- Laibson, D., & List, J. A. (2015). Principles of (behavioral) economics. *American Economic Review*, *105*(5), 385-390. http://www.jstor.org/stable/43821914.
- Leuba, J. H. (1912). The varieties, classification, and origin of magic. *American Anthropologist*, *14*(2), 350-367. https://www.Jstors.org/stable/659937.
- Lombard, M. (2005). “A Method for Identifying Stone Age Hunting Tools: *The South African archeologicalBulletin.* South African Archiological Society, *60*, 182 - 202. Inapatikana katika https://www.org.Jstor/stable/2889126.Imesomwa tarehe 4/12/2022.
- Mahmood, W. S. (2020). “Fantasy in Children Literature.” *Journal of Arts, Literature, Humanities and Social Sciences*, 59, 452 - 465. Inapatikana

katika www.Jalhass.com. Imesomwa tarehe 30/10/ 2022.

- Mariki, F. (2004). *Hadithi ya Morile*. Dar es Salaam: Mkuki Na Nyota Publishers Ltd.
- Mbiti, J. S. (1969). *African Religions & Philosophy*. Nairobi: East African Education Publishers.
- Moshi, R. (1995). *Sinderela.* Dar es Salaam: Mture Publishers Limited.
- Mzindakaya, C. (2005). *Hadithi za Kusisimua*. Dar es Salaam: HEKO Publishers Ltd.
- Panegyres, K. (2016). Notes on a Nestorian Spell against Headaches. *Mnemosyne*, *69*(3), 491-502. http://www.jstor.org/stable/24772060.
- Rowe, M. (2000). Stickers for nails: The ongoing transformation of roles, rites, and symbols in Japanese funerals. *Japanese Journal of Religious Studies*, 353-378. http://www.jstor.org/stable/30233670. Imesomwa tarehe 10/3/2023.
- Semzaba, E. (2008). *Marimba ya Majaliwa*. Dar es Salaam: E&D Vision Publishing.
- Stökl, J. (2014) "Divination as Warfare: The Use of Divination across Borders in J. Stökl & A. Lenzi (Eds.) *Divination, Politics, and Ancient Near Eastern Empires."* Society of Biblical Literature, 49 - 64). Inapatikana katika https://doi.org/10.2307/j.ctt1287n4q.6. Imesomwa tarehe 11/1/2023.
- Subbotsky, E. (2010). *Magic and the mind: Mechanisms, functions, and development of magical thinking and behavior*. Oxford University Press. https://w.w.w.researchgat.net/publication/261595945. Imesomwa tarehe 20/10/2022.
- Sullivan, C. W. (1997). Jumping the broom: A further consideration of the origins of an African American Wedding Custom. *Journal of American folklore*, *110*(436), 203-204. https:/www.jstor.org/stable/541813. Imesomwa tarehe 4/12/2022.
- TUKI. (2004). Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Nairobi: Oxford University Press.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi : Focus Publicational ltd.
- Whiteley, N. (1987). 'SEMI-WORKS OF ART': CONSUMERISM, YOUTH CULTURE AND CHAIR DESIGN IN THE 1960S. *Furniture History*, *23*, 108-126. http://www.Jstor.org/stable/2340670.
- Wolff, M. A. (2010). "What Is Changing? The Future Is Not What It Used to Be." *Federal Sentencing Reporter*, 23(2), 150-152. https://doi.org/10.1525/fsr.2010.23.2.150.

**Cite This Article:** Gloria Kimbi, Dkt, Edith Lyimo, Dkt, Grace Minja (2024). Ubainifu WA Matendo Ya Kisihiri: Mifano Kutoka Bunilizi Teule Za Fasihi Ya Kiswahili Ya Watoto. *East African Scholars J Edu Humanit Lit*, *7*(2), 59-68.